

TANGAZO LA SERIKALI NA. 588 la tarehe 30/9/2022

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

SHERIA NDOGO ZA (AFYA, USAFI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA) HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE, ZA MWAKA 2022

Jina	1.	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, za Mwaka 2022.
Matumizi	2.	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.
Tafsiri	3.	Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:- “ Ada ” maana yake ni malipo yanayotakiwa kulipwa Halmashauri na kampuni, viwanda, mtu binafsi, taasisi kwa ajili ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri “ Ada ya uchafuzi wa Mazingira ” maana

	<p>yake ni malipo yanayotakiwa kulipwa kwa Halmashauri na kampuni, viwanda, kikundi, mtu binafsi na taasisi ambazo shughuli zao zinasababisha uchafuzi wa mazingira; kwa kuzingatia kanuni ya mchafuzi hulipa (Polluter Pay Principle (PPP).</p> <p>“Adha” maana yake hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu na viumbe hai kwa ujumla;</p> <p>“Afya” maana yake hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala sio tu kutokuwa na ugonjwa au kilema;</p> <p>“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;</p> <p>“Bafu” maana yake chumba maalum kilichojengwa kwa madhumuni ya kuogea.</p> <p>“Chakula” maana yake kitu chochote kinacholiwa na binadamu na inajumuisha maji na dawa;</p> <p>“Chanzo cha maji” maana yake ni eneo lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii ikiwemo visima, mito, chemchemi, vijito, na maeneo yote yanayopatikana maji;</p> <p>“Chemba ya ukaguzi” maana yake ni sehemu maalum iliyotengenezwa kwa ajili</p>
--	--

	<p>ya ukaguzi wa mfereji ambao una mfuniko usioruhusu hewa kutoka;</p> <p>“Choo bora” maana yake ni choo cha lindi chenye shimo lililojengwa madhubuti au choo chochote cha maji chenye sakafu imara, banda imara la kudumu, imezekwa, kina mlango imara kama cha lindi kimeongezwa bomba la kutoa hewa chafu na chenye mfuniko kwenye tundu la choo;</p> <p>“Chukizo la Afya” maana yake kitu chochote kinachoweza kuleta kinyaa machoni kwa kuona, kunusa, hewa chafu, madhara au kuhatarisha Afya za binadamu na wanyama;</p> <p>“Duka Genge” maana yake ni duka ambalo uhusisha uuzaji wa mchanganyiko wa bidhaa na matunda, mboga mboga, vyakula na bidhaa nyingine za madukani;</p> <p>“Genge” maana yake ni biashara inayohusisha uuzaji wa bidhaa hususani matunda na mboga mboga;</p> <p>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke;</p> <p>“Hati ya Usafi” maana yake ni hati inayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi na Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka</p>
--	--

	<p>2012 na kanuni zake;</p> <p>“Hifadhi ya Mazingira” maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji kwa kuzingatia masharti na maelekezo ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine zinazohusu utunzaji wa mazingira;</p> <p>“Jengo la Biashara” maana yake jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na mamlaka kufanya biashara iliyokusudiwa;</p> <p>“Kaya” maana yake mtu mzima anayejitgemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye maeneo ya Kata za Halmashauri;</p> <p>“Kelele” maana yake ni kero isababishwayo na sauti ambayo kwa asili inakataliwa au ile ambayo inaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu au mazingira,</p> <p>“Kikundi cha usafishaji” maana yake kikundi chochote cha watu kilichosajiliwa kufanya shughuli za usafi wa mazingira na hasa za udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri;</p> <p>“Kizimba cha taka” maana yake ni kizimba cha taka au chombo maalum kilichowekwa na Halmashauri kwa ajili ya</p>
--	---

	<p>jamii kuhifadhia taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye jalala kuu lililoidhinishwa;</p> <p>“Kituo cha taka” maana yake kizimba cha taka au chombo maalum cha kuhifadhia taka, kasha “refuse bin container” ambayo imewekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya Jamii inayoishi jirani kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye jalala la taka ngumu la Halmashauri;</p> <p>“Kuchakata Taka” maana yake ni kuzichambua, kuzitenganisha na kuzibadili kuwa kitu kingine chenye manufaa kwa jamii;</p> <p>“Kutupa taka ngumu” maana yake ni kukusanya taka zote zinazozalishwa na kaya, kampuni, sehemu ya biashara, ofisi, taasisi, ofisi ya serikali na binafsi n.k na kuzipeleka hadi kwenye jalala kuu la Halmashauri kwa madhumuni ya kuzitupa kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na Halmashauri;</p> <p>“Mabwawa ya maji taka” maana yake ni mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutakasa maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kutoka</p>
--	--

	<p>vyooni, kutoka bafuni, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote za nyumbani na viwanda;</p> <p>“Magonjwa ya mlipuko” maana yake ni magonjwa yanayotokea kwa muda mfupi ya kuambukiza na kuenea kwa haraka na kuathili watu wengi ndani ya muda mfupi yanayoweza kutolewa amri ya taadhari, kupooza, kipindupindu, kuhara, louse bare typhus, (relapsing) fever, surua na homa ya matumbo;</p> <p>“Mkazi” maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri, ambaye anamiliki kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;</p> <p>“Mazalio ya wadudu” maana yake ni sehemu ambayo wadudu hufanya mazalio au kuishi kwa minajiri ya kufanya mzunguko wa maisha na baadae huleta maadhara kwa binadamu;</p> <p>“Mifugo” maana yake ng’ombe, punda, nguruwe, mbuzi, kondoo au kuku na wanyama wengine wote wafugwao majumbani;</p> <p>“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi;</p>
--	---

	<p>“Mzalishaji wa taka ngumu” maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara au kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake za kila siku huzalisha taka ngumu;</p> <p>“Mtandao wa maji taka” maana yake mfumo wa bomba kuu lililojengwa kwa madhumuni ya kupokea na kusafirisha taka miminika toka kwenye mifereji ya maji na kuyapeleka kwenye mabwawa ya maji taka au baharini;</p> <p>“Mzalishaji wa maji taka” maana yake mtu, shirika, kiwanda au taasisi ambapo shughuli zake kwa namna yoyote ile huzalisha maji taka;</p> <p>“Nyumba za makazi” maana yake ni jengo lolote linalotumiwa kwa kuishi, na inajumuisha ardhi inayozunguka jengo husika;</p> <p>“Pipa la taka” maana yake chombo chochote kilichokubaliwa na Halmashauri kitumike kama chombo cha kuhifadhia taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini, pamoja na chombo maalum kinachobebwa na gari la takataka;</p> <p>“Taka ngumu” maana yake kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani yoyote kwa jamii inayohusika,</p>
--	--

	<p>uwepo wake katika eneo husika unaweza kusababisha machukizo ya kiafya na kuhatarisha afya ya jamii;</p> <p>“Taka za majumbani” maana yake mabaki ya vyakula, maganda ya matunda, majivu, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali, kinyesi cha mifugo, taka za bustani na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;</p> <p>“Taka ndogo ndogo” maana yake mabaki ya vocha za simu, chupa za maji, chupa za juisi, maganda ya pipi, chocolate, ice cream, pakiti za sigara, vichungi vya sigara, vizibo vya chupa, maganda ya matunda, miwa, mahindi, machungwa, mananasi, masalia ya magunzi, mbogamboga, magazeti na karatasi za aina mbalimbali, na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;</p> <p>“Taka za biashara” maana yake ni aina yoyote ya taka ambazo hupatikana au hutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara;</p> <p>“Taka za viwanda” maana yake aina yoyote ya taka ambazo hutokana na uzalishaji wa shughuli mbalimbali viwandani;</p> <p>“Taka hatari” maana yake aina yoyote ya taka ambayo kwa njia fulani hubaki kwenye mazingira na hatima yake ni kusababisha madhara kwa afya ya jamii</p>
--	--

	<p>ikiwa ni pamoja na taka zitokanazo na shughuli za hospitali, shughuli za mionzi “X –ray, films, radio active materials”, vitu vyenye ncha kali kama sindano, chupa au taka zitokanazo na shughuli za uzalishaji viwandani kama vile (dry batteries), mercury, madawa mbalimbali, mabaki ya vyuma, kemikali, gesi mbalimbali;</p> <p>“Taka miminika” maana yake maji yaliyokwisha tumika au chafuliwa kwa namna yoyote ile ambayo yanajumuisha maji machafu toka chooni, bafuni, jikoni, viwandani, maji yaoshewayo vyombo, maji yaliyofuliwa nguo, kuosha nywele, kuoshea vyakula na yaliyopigiwa deki;</p> <p>“Ufugaji wa afya” maana yake ufugaji ndani ya eneo lililoruhusiwa na si nje ya banda au jingo.</p> <p>“ Uchunguzi wa afya” maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vya Magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi;</p> <p>“Ugonjwa wa kuambukizwa” maana yake ugonjwa wowote uambukizwao toka kwa mtu na mtu au mtu kwa mnyama, mtu kwa mdudu mfano kifua kikuu, brucellosis, kimeta, safura, surua, kipindupindu au uti wa mgongo n.k.</p>
--	---

Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>“Wafanyabiashara wadogo (wamachinga)” maana yake ni wafanyabiashara wadogo ambao wanatembeza biashara zao kwenye maeneo mbali mbali yenye wateja/watu;</p> <p>“Wakala” maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, Kampuni au Shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri;</p>
Mamlaka ya Halmashauri	4.	<p>(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukagua nyumba yoyote, kiwanja, barabara, njia au uchochoro, mfereji wa maji ya mvua au Ardhi yoyote katika eneo lolote la Halmashauri muda wowote na kuchukua hatua zozote itakazoonza zinafaa katika kuweka mazingira kuwa kwenye hali ya usafi.</p> <p>(2) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote anayekiuka Sheria Ndogo hizi au sheria nyingine zinazohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira nchini.</p> <p>(3) Kutoza ada, faini, fidia na kufifilisha kosa.</p> <p>(4) Kuteua mtu yeyote, wakala, kikundi au taasisi kutekeleza shughuli za usimamizi wa afya, usafi wa mazingira kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria ndogo hizi.</p>
Wajibu wa kila mkazi au mfanyabiashara	5.	<p>(1) Ni wajibu wa kila mkazi au</p>

		<p>mfanayabiashara anayemiliki jengo au eneo la biashara kuhakikisha kwamba:-</p> <ul style="list-style-type: none">(a) majani yanayozunguka jengo lake au makazi yanakatwa au kupaliliwa na kuondolewa katika eneo lake lote.(b) takataka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri.(c) maji taka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa maji taka (sewage system).(d) kuboresha na kupaka rangi jengo lake kila inapochakaa.(e) kuwa na choo kilicho bora na kisafi wakati wote.(f) atashiriki siku ya usafi ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi.(g) ataondoa uchafu ikiwemo mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo katika mfereji wa maji ya mvua inayomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa
--	--	---

		<p>safi wakati wote.</p> <p>(h) atatakiwa kuweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.</p> <p>(i) kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuathiri upitishaji wa maji ya mvua na hivyo kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla.</p> <p>(j) anafanya uchambuzi wa taka (sorting).</p> <p>(2) Ni wajibu wa kila mfanyabiashara wa matunda au miwa kuhakikisha kuwa ana chombo maalumu cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.</p> <p>(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji dawa au biashara ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na awe amelipia ada ya kibali kutoka Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.</p>
--	--	--

Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		(4) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kutupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.
Wajibu wa Halmashauri kusimamia vyanzo vya maji	6.	(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa:- (a) kusimamia na kulinda vyanzo vya maji. (b) kuchukuwa hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji, kuchafua chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi. (c) Kupanda miti isiyonyonya maji taka katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu.
Ada ya uzoaji taka	7.	Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira kama ilivyoordheshwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.
Kukusanya ushuru bila kibali	8.	Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukusanya ushuru wa taka ngumu bila kibali.

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

Muda wa mwisho wa kulipa ushuru	9.	Muda wa mwisho wa kulipa ushuru wa taka ngumu ni tarehe tano ya mwezi unaofuata. Baada ya hapo ushuru utalipwa pamoja na adhabu ya 20% ya ushuru uliotakiwa kulipwa.
Kusudio la sheria	10.	Halmashauri itahakikisha kunakuwa na kiwango cha juu cha udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na kupunguza machukizo ya kiafya katika maeneo yote ya Halmashauri na hivyo kufanikisha uwepo wa mazingira safi na salama.
Wajibu wa kuwa na pipa la takataka	11.	(1) Kila kaya iliyoko ndani ya Halmashauri inatakiwa kuwa na pipa lenye mfuniko litakalotumika kutupia taka ngumu. (2) Chombo chochote kilichobeba taka ngumu kinatakiwa kiwe kimefunikwa kiasi cha kuzuia taka ngumu zisionekane wala kumwagika chini na kuleta adha kwa watu na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla.
Kibali cha matengeezo ya vyombo vya moto	12.	(1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa na kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri baada ya kulipia ada au ushuru. (2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote:- (a) kutengeneza gari, pikipiki au

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.</p> <p>(b) kuegesha magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mitaro, maeneo ya wazi au barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.</p> <p>(c) kumwaga ovyo au kutiririsha oil, mafuta machafu na grisi maeneo yasiyoruhusiwa.</p> <p>(d) kufanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.</p>
Udhibiti wa kelele	13.	Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kusababisha au kufungulia kelele kupita kiasi bila kupata kibali cha Afisa Mwidhiniwa.
Makosa yatokanayo na vyanzo vya maji	14.	<p>Ni kosa kwa mtu yeyote:-</p> <p>(a) kunawa, kuoga, kufulia nguo au kunywesha mifugo karibu au kwenye chanzo cha maji kama vile</p>

		<p>chemchem, kisima au chanzo kingine chochote cha maji.</p> <p>(b) kujenga boma la mifugo karibu au kuruhusu mkojo ya mifugo au maji machafu kuelekea karibu na chanzo cha maji.</p> <p>(c) kufuga mifugo ya aina yoyote bila kibali cha Halmashauri au kuachia mifugo au kusababisha kuzurura ovyo mtaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.</p> <p>(d) kuanzisha na kufanya shughuli za aina yoyote ndani ya mita 60 katika maeneo yote oevu na chepechepe na maeneo yote kama ukanda wa kijani.</p> <p>(e) kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kujenga, kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.</p> <p>(f) kumiliki eneo la chanzo cha maji asili isipokuwa Halmashauri.</p> <p>(g) kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya</p>
--	--	---

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.</p> <p>(h) kuunganisha maji ya mvua na maji taka au kutapisha choo na kutiririsha vinyesi vya mifugo au binadamu kwenye chanzo cha maji au mfereji wa maji ya mvua.</p> <p>(i) kuweka kitu chochote chenye sumu kwenye chanzo cha maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote chenye uhai.</p>
<p>Udhibiti wa utupaji taka ovyo</p>	<p>15.</p>	<p>(1) Ni marufuku kutupa taka ovyo katika maeneo ya makazi, biashara au mahali popote pasipotengwa kwa ajili ya kutupa taka.</p> <p>(2) Ni wajibu wa kila mtu, muda wowote akiwa ndani ya Halmashauri, kuhakikisha kuwa anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunza taka katika maeneo rasmi yaliyotengwa.</p> <p>(3) Ni marufuku kwa watumiaji wa gari binafsi au basi la abiria kutupa taka nje ya gari</p> <p>(4) Mabasi ya abiria ni lazima yawe na chombo/vyombo cha kuhifadhi taka na pia kuwe na maandishi yanayoonekana wazi yanayowaonya abiria kutotupa taka nje ya</p>

Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>basi.</p> <p>(5) Ni wajibu wa kila mkazi au mtu yeyote kutunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vilivyowekwa na Halmashauri.</p> <p>(6) Mmiliki wa gari binafsi au basi la abiria atakuwa na wajibu wa kukusanya na kutupa taka katika eneo lililotengwa kwa ajili ukusanyaji na uzoaji wa taka maeneo ya vituo vya daladala.</p>
Kutiririsha maji taka	16.	<p>(1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kutiririsha au kumwaga au kuruhusu au kusababisha kutiririsha au kumwaga maji taka barabarani, uchochoroni kwenye mifereji, mtoni, kwenye vyanzo vya maji au sehemu yoyote isiyotengenezwa kuhifadhi maji taka.</p> <p>(2) Itakuwa ni wajibu wa kila kiwanda kinachozalisha maji taka kuhakikisha kuwa kinaunganisha maji taka au kujenga mifereji na mabwabwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka ya kiwanda.</p> <p>(3) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo la kuhifadhi linapojaa na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha karo kujaa na kutiririsha maji taka barabarani au sehemu yoyote isiyoruhusiwa.</p>

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

Uchambuzi wa Taka	17.	<p>(1) Taka zote zitapaswa kuchambuliwa sehemu zinakotoka katika makundi ya taka zenye madhara na zisizo na madhara ili kuwezesha utofauti na kurahisisha usimamizi, usafirishaji na utupaji wake.</p> <p>(2) Taka zote zilizo na madhara zitatumzwa kwenye chombo cha rangi nyekundu kilichowekewa alama ya “Taka hatarishi”.</p> <p>(3) Taka zote zenye ncha kali zitatumzwa au kuwekwa kwenye mifuko ya pekee na kuwekwa alama ya kutoa tahadhari; “Hatari Usifungue”.</p> <p>(4) Taka zote zinazohusiana na taka rejea (Recycling) zitachambuliwa na kuwekwa kwenye vyombo maalum vitakavyoelekezwa na Afisa Mwidhiniwa.</p>
Taka za viwanda	18.	<p>(1) Ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya, vumbi au kelele na kusababisha kero kwa wakazi.</p> <p>(2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.</p> <p>(3) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine</p>

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.
Taka hatarishi	19.	Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote, kampuni, wakala au taasisi kuendesha shughuli za uchomaji wa taka hatarishi bila ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.
Usalama wa maji ya kunywa	20.	Ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.
Usalama wa maji ya visima	21.	Ni wajibu wa kila mmiliki wa kisima kuhakikisha maji ya kisima yamepimwa ili kujua kama ni salama kwa matumizi.
Utengenezaji na uuzaji vyakula	22.	Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha na kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya.
Uuzaji vyakula vilivyopikwa	23.	Ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia inzi, vumbi na

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.
Usalama wa vyakula	24.	(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza. (2) Ni marufuku kupanga vyakula nje ya duka la vyakula
Uzuiaji wa shughuli wakati wa Magonjwa ya mlipuko	25.	Mkurugenzi anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.
Ukamataji wakati wa zuio	26.	(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kumkamata mtu yeyote ambaye atakaidi amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko. (2) Endapo mtu aliyekamatwa alikuwa anauza vyakula ambavyo vinaharibika kwa haraka Halmashauri itaharibu vyakula hivyo. (3) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1) na (2), endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka Halmashauri itakuwa na jukumu la

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.</p> <p>(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.</p>
<p>Machinjio na maduka ya nyama</p>	<p>27.</p>	<p>(1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakikisha kwamba duka lake:-</p> <p>(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa kuweka sakafuni na ukutani marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu.</p> <p>(b) lina maji safi na misumeno ya kukatia nyama.</p> <p>(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu za mizani.</p> <p>(d) lina pipa la kuhifadhia taka taka.</p> <p>(e) lina mavazi maalum kwa ajili ya kuendeshea biashara ikiwemo aproni, mabuti meupe na kofia.</p> <p>(2) Muuzaji yeyote wa nyama atatakiwa kuvaa vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe na sharti awe anapima afya kila baada ya miezi sita.</p>

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa	28.	Ni kosa kwa mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.
Matumizi ya vyoo bora	29.	<p>(1) Kila mmiliki wa nyumba za kuishi katika eneo la Halmashauri anatakiwa kuwa na choo bora na safi kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo.</p> <p>(2) Kila mmiliki wa nyumba inayotumika kwa shughuli za ibada, biashara, hoteli, mgahawa, nyumba ya kulala wageni, baa, klabu, gereji au shughuli yoyote inayokusanya watu wengi kwa pamoja anatakiwa kuweka na kutunza vyoo vya kutosha kwa jinsia za kiume na kike.</p> <p>(3) Kila mwenye nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa choo chake ni kisafi na kinafanyiwa usafi kila siku, kupulizwa dawa ya kua wadudu mara kwa mara na kunyonywa uchafu au majitaka pale kinapojaa kama choo ni cha shimo.</p> <p>(4) Iwapo itagunduliwa kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo hakifai kwa matumizi ya binadamu, Halmashuri itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua yoyote inayoona inafaa ikiwa ni pamoja na kuzuia nyumba hiyo isitumike hadi choo kitakapojengwa au kukarabatiwa.</p>
Uwezo wa kukagua	30.	(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa saa za kazi na wakati wowote inapotakiwa kufanyika kwa ukaguzi maalumu kukagua utekelezaji wa

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.</p>
Vyoo vya umma	31.	<p>(1) Halmashauri inaweza kujenga choo cha Umma au kumruhusu mtu binafsi, kikundi au taasisi kujenga vyoo vya Umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa.</p> <p>(2) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi vitatakiwa viwe vya kudumu na:-</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) matundu yasiyopungua mawili (2) kwa wanawake na mawili (2) kwa wanaume. (b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama. (c) kuwepo na chombo cha kuhifadhia maji ya akiba. (d) kuwepo kwa bafu ya wanaume na wanawake. (e) kuwepo na chumba maalumu cha kuvutia sigara. (f) kuwepo na eehemu ya haja ndogo kwa wanaume. (g) kuwepo na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.
Vyoo vya muda katika mikusanyiko	32.	Ni wajibu wa mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		madhumuni ya mkutano au sherehe au mkusanyiko wowote kuweka au kujenga vyoo vya muda endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu na atatakiwa kuomba idhini kutoka Halmashauri.
Kujisaidia eneo ambalo siyo choo	33.	Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kujisaidia haja kubwa au ndogo katika eneo ambalo siyo choo.
Ilani ya kuondoa kero	34.	(1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ndani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo. (2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.
Eneo maalum la uvutaji sigara	35.	(1) Ni kosa kwa mtu yeyote kuvuta sigara kwenye eneo la wazi au kwenye mikusanyiko ya watu. (2) Kila mwenye jengo la biashara za baa, hoteli, mgahawa, kumbi za starehe, viwanja vya michezo na burudani, Ofisi za umma na binafsi anatakiwa kutenga eneo maalum la kuvutia sigara na kuweka chombo cha kuhifadhia majivu na vichungi vya sigara.
Uanzishaji na Utunzaji wa Bustani za maua	36.	(1) Halmashauri itaratibu shughuli za uanzishaji na utunzaji wa Bustani za maua katika maeneo ya wazi, kingo za barabara na maeneo mengine kadri itakavyoona inafaa ili kuweka mandhari nzuri na kupendezesha Manispaa.

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>(2) Mkurugenzi anaweza kutoa kibali kwa mtu yeyote, taasisi, kikundi binafsi au asasi ya kiraia, ndani ya Halmashauri katika ngazi ya Mtaa, Kata au Wilaya katika kuboresha bustani, eneo la wazi, kusimamia uhifadhi na usimamizi wa mazingira.</p> <p>(3) Kila Mmiliki wa Ardhi au Nyumba au Jengo atawajibika kupendzesha mazingira na mandhari ya eneo lake, kuzunguka makazi yake kwa kupanda maua na kuyatunza.</p>
Usafi na Utunzaji wa Fukwe	37.	<p>(1) Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itakuwa na wajibu wa kutunza na kusafisha fukwe zilizopo ndani ya Halmashauri.</p> <p>(2) Mtu yoyote hataruhusiwa kufanya shughuli za biashara ya aina yoyote katika maeneo ya fukwe bila kibali cha Halmashauri.</p> <p>(3) Mmiliki wa nyumba au hoteli iliyo karibu na fukwe hataruhusiwa kutiririsha maji machafu au kutupa taka ya aina yoyote katika maeneo ya fukwe au Baharini.</p>

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

Makosa yatokanayo na uharibifu au uchafuzi wa bahari na rasilimali zake	38.	<p>Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> (a) atatumia juva, baruti, sumu au makuki kuvua. (b) atavua kwa kutumia nyavu (ring net) kwenye maji mafupi au kwenye miamba. (c) atavua, kuokota, kuchukua au kufanya kitendo chochote kwenye maeneo tengefu ya samaki isipokuwa kwa kibali maalumu cha Mkurugenzi. (d) atavua samaki bila kuwa na leseni ya uvuvi. (e) atatumia chombo cha uvuvi kisichokuwa na namba za usajili pamoja na leseni ya chombo hicho. (f) atafanya biashara, kupiga picha kwenye ufukwe bila kibali cha Mkurugenzi.
Udhibiti wa Hewa ya Ukaa	39.	<p>Halmashauri kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, Wadau na Makampuni binafsi itafanya, itasimamia na kudhibiti viwango vya uzalishaji wa Hewa ya Ukaa kutoka katika vyombo vya uzalishaji, vyombo vya moto kama vile mabasi, magari ya mizigo, magari madogo na pikipiki kwa kuvipima viwango vya uchafuzi wa mazingira na kuchukuwa hatua pale ambapo kiwango cha uchafuzi kitazidi kile kinachokubalika kisheria.</p>

Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

Udhibiti wa mifugo mjini	40.	<p>(1) Itakuwa kosa kwa mtu yeyote kufuga mfugo wa aina yoyote bila kuomba na kupata kibali cha Halmashauri.</p> <p>(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuachwa kuzurura ovyo mtaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.</p> <p>(3) Mfugo wowote utakaokutwa ukizurura au kuchungwa kwenye eneo lisiloruhusiwa utakamatwa na Halmashauri na mwenye mfugo atalazimika kulipa faini na fidia kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na sheria nyingine za nchi.</p>
Upandaji na utunzaji wa miti	41.	<p>(1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukata mti wa aina yoyote bila kibali cha Halmashauri.</p> <p>(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mwenye nyumba katika eneo la Halmashauri kupanda na kutunza miti ya kivuli au matunda katika eneo lake kwa ujazo ulioanishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.</p>
Upimaji wa afya	42.	<p>(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mhadumu wa hoteli, migahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza kupima Afya zao kila baada ya miezi sita.</p> <p>(2) Itakuwa ni kosa kwa mmiliki yeyote kuruhusu mhadumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake.</p>

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

Taarifa za mgonjwa	43.	Itakuwa ni wajibu wa kila mtu kutoa taarifa ya uwepo mgonjwa au magonjwa ya mlipuko katika eneo lake.
Uchimbaji na usafirishaji wa kokoto	44.	<p>(1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuchimba kokoto, mawe au mchanga katika eneo la Halmashauri bila kibali cha maandishi cha Halmashauri.</p> <p>(2) Mtu yeyote anayetaka kuchimba mchanga, kokoto au mawe katika eneo la Halmashauri atatakiwa kutuma maombi yake kwa maandishi na kulipa ada ya maombi hayo kwa viwango vilivyopangwa na Halmashauri.</p> <p>(3) Halmashauri itatoza ushuru wa mchanga, kokoto au mawe kutoka kwa kila mtu anayesafirisha Madini ya ujenzi katika eneola Halmashauri.</p> <p>(4) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukataa maombi yoyote iwapo itaona kuwa uchimbaji wa kokoto, mawe au mchanga utasababisha uharibifu wa mazingira.</p> <p>(5) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri kuhakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha mchanga, mawe au kokoto kimefunikwa ili kuzuia mchanga, kokoto au mawe kumwagika na kuchafua mazingira.</p> <p>(6) Chombo chochote kitachotumika kusafirisha mawe, mchanga au kokoto kinyume na Masharti ya kifungu kidogo cha (5) kitakamatwa na mmiliki wake atalipa faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kama gharama za uchafuzi wa</p>

Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>mazingira kabla ya gari hiyo kuachiwa.</p> <p>(7) Iwapo gharama hiyo haitalipwa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya kukamatwa chombo hicho Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuuza kwa njia ya mnada baada ya kuomba na kupata kibali cha Mahakama ili kufidia gharama hizo na kiasi kitakachobaki atarudishiwa mmiliki wa chombo.</p>
Wajibu wa Wakala	45.	<p>Wakala atakayeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-</p> <p>(1) Kukusanya, kwa niaba ya Halmashauri, ada mbalimbali zinazohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira, katika eneo lake alilopangiwa na kwa viwango vilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Wakala atakusanya ada kwa kutumia mfumo wa kielekitroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.</p> <p>(3) Atatekeleza yote yaliyomo kwenye mkataba.</p>
Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa	46.	<p>Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa:-</p> <p>(1) Kusimamia uanzishwaji, usimamizi na kushauri kuhusu namna bora ya kutunza na kutupa taka kwa kushirikiana na Mamlaka husika.</p> <p>(2) Wakati wowote atakaona unafaa kuingia katika jengo au sehemu yoyote</p>

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		<p>kwa nia ya kukagua uzalishaji na udhibiti wa taka au kutoa maagizo ya namna ya ukusanyaji, uandaaji na uchakataji wa taka kulingana na aina ya taka.</p> <p>(3) Kutoa maelekezo namna ya kuhifadhi, kuchambua, kutupa au kuharibu taka zilizokusanywa kutoka katika maeneo yote.</p>
Makosa ya jumla	47.	<p>Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-</p> <p>(1) Atamzuia au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Atamwaga taka barabarani, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa.</p> <p>(3) Ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi.</p> <p>(4) Atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani.</p> <p>(5) Ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu.</p> <p>(6) Atapika vyakula pembezoni mwa barabara au nje ya majengo mengine.</p>

		<p>(7) Atauza vyakula maeneo yasiyo rasmi na kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo.</p> <p>(8) Atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji.</p> <p>(9) Atavuta sigara hadharani au mahali pa jumuiya au kwenye vyombo vya usafiri.</p> <p>(10) Atatema mate ovyo au kutema mate barabarani au mahali pa jumuiya.</p> <p>(11) Ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu.</p> <p>(12) Ataacha nyumba anayoishi au kumiliki au kufanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo.</p> <p>(13) Ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji.</p> <p>(14) Ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi.</p> <p>(15) Ataenda haja ndogo au kubwa</p>
--	--	--

		<p>ovyo barabarani, uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni.</p> <p>(16) Atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.</p> <p>(17) Kuteketeza taka kwa kuchoma moto, au kufukia ardhini bila kibali cha Halmashauri.</p> <p>(18) Kufanya biashara au maonyesho ya biashara yoyote au shughuli nyingine yoyote katika maeneo ya karibu au ndani au juu ya mifereji au mitaro ya maji, au katika maeneo ya kukusanyia.</p> <p>(19) Itakuwa marufuku kwa mtu yeyote kunywaga maji ya betri kwenye ardhi chanzo cha maji, n.k.</p> <p>(20) Ni marufuku mtu yeyote kukusanya na safirisha betri zilizotumika kama betri za magari, solar, simu na solar panel bila kuwa na kibali toka ofisi ya Makamu wa Rais;</p> <p>(21) Itakuwa marufuku kuzalisha,</p>
--	--	--

Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		kusambaza na kutumia mifuko ya plastiki.
Kufanya tathmini ya mazingira	48.	<p>(1) Miradi yote inayotekelezwa ndani ya Halmashauri haitoendelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira.</p> <p>(2) Kila mpendekezaji wa mradi atawajibika kulipa Halmashauri asilimia kumi (10%) ya gharama ya tathmini ya athari za mazingira kama ada ya ukaguzi na usimamizi wa mradi husika.</p>
Makosa	49.	<p>Ni kosa kwa mtu yeyote:-</p> <p>(1) Kuchoma moto kwa namna yoyote ile katika maeneo yaliyoko eneo la Halmashauri.</p> <p>(2) Kuchoma moto taka ndani ya eneo la Halmashauri.</p> <p>(3) Kuandaa shamba kwa njia ya kuchoma moto.</p> <p>(4) Kuchafua anga hewa “Air Pollution” kwa kuachilia moshi angani unaoweza kuleta madhara kwa binadamu, mimea na viumbe hai.</p> <p>(5) Kukata miti katika eneo la Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali.</p> <p>(6) Kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe</p>

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

		maalumu ambao ni rasilimamli ya Taifa.
Adhabu	50.	Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (Tshs. 300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.
kufifilisha kosa	51.	Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari yake mwenyewe kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na kulipa faini ya kiasi cha shilingi laki mbili (200,000.00).
GN. No 310 /2010	52.	Sheria Ndogo za (Udhibiti wa uchafuzi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, GN. No 310 ya 27/08/2010 zimefutwa.

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 7)

Ada ya Uzoaji wa Taka Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Na	Aina ya mzalishaji taka	Kiwango cha ada kwa mwezi (Tshs.)
1.	Nyumba za makazi (Kwa kaya)	3,000
2.	Nyumba ya makazi ghorofa moja (Kwa kaya)	10,000
3.	Nyumba za makazi zaidi ya ghorofa moja (Kwa kaya)	15,000
4.	Nyumba kubwa ya pekee (Bungalow) (Kwa kaya)	15,000
5.	Hostel (kwa chumba)	3,000
6.	Nyumba ya kulala wageni (Guest house)	50,000
7.	OFISI	30,000
8.	Tawi la Benki ya biashara	100,000
9.	Duka la kubadilishia fedha	60,000
10.	Ofisi za ATM	60,000
11.	Ofisi za luku (Tanesco)	60,000
12.	Ofisi za luku (wakala)	30,000
13.	Mawakala wa fedha kwa mitandao ya simu na benki	30,000
14.	Soft drinks (Vinjwaji laini)	20,000
15.	Sehemu ya kutengenezea chai na vitafunwa (tearoom, snacks & soft drinks)	20,000
16.	Cafe/Restaurant (food/snacks & soft drinks)	120,000
17.	Duka la vyakula na vinywaji (Grocery)	15,000
18.	Baa (pombe, vinywaji baridi na vitafunwa)	30,000
19.	Mama na baba lishe	15,000
20.	Vilabu vya pombe za kienyeji	20,000
21.	Vibanda vya chips	15,000
22.	Baa na mgahawa/jiko	60,000
23.	Wauza madafu	60,000
24.	Baa na nyumba ya kulala wageni (Bar&Guest house)	100,000
25.	Baa, nyumba ya wageni na Ukumbi wa starehe	200,000
26.	Baa na ukumbi wa starehe	150,000
27.	Baa, Ukumbi wa starehe na mgahawa	200,000
28.	Ukumbi wa starehe	100,000

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

29.	Duka la kuuza Ice Cream	100,000
30.	HOTEL&LODGE	200,000
31.	Bucha ya nyama na /au samaki wabichi	20,000
32.	Vyakula/bidhaa mchanganyiko	30,000
33.	Duka la nguo	20,000
34.	Vifaa vya umeme au simu (Electronic phone, phone accessories and electrical appliances)	40,000
35.	Vifaa vya ujenzi Hardware/ Machinery	80,000
36.	Vitabu/ Shajala (Stationaries)	20,000
37.	Urembo/ Vipodozi	20,000
38.	Duka la Samani (Furniture and Machinery)	40,000
39.	Vinywaji na Pombe Kali (beverages and liquor stores)	30,000
40.	Taka zinazotokana na ghala la kuhifadha bidhaa (Store)	50,000
41.	Vipuri na Vifaa (Spare parts and tools)	20,000
42.	Duka la vifaa chakula	20,000
43.	Fundi Seremala	60,000
44.	Karakana ya Chuma (Metal W/shops)	50,000
45.	Karakana ya Magari (Motor Garage)	50,000
46.	Sonara na uhunzi wa vito (Jewelry and Black Smith)	15,000
47.	Shughuli za Vioo (Glass Works)/ Shughuli za Alminium	50,000
48.	Mchapishaji (printing)	100,000
49.	Mashine ya mbao kwa ujazo wa mita moja saw mill per m ³	15,000
50.	Umeme na Matengenezo ya elektroniki (Electronical and Electronic repair)	25,000
51.	Magurudumu na matengenezo	30,000
52.	Fundi cherehani	20,000
53.	Fundi viatu (cobler/ Shoe repair)	3,000
54.	Saluni ya nywele za kike	10,000
55.	Saluni ya nywele za kiume	10,000
56.	Dobi and dry cleaner	10,000
57.	Genge kwa meza moja	5,000
58.	Wauza matunda na juisi nyinginezo	20,000
59.	Huduma za Intenet	10,000
60.	Duka la dawa baridi	10,000

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

61.	Pharmacy	10,000
62.	Duka la dawa rejereja (Retail)	20,000
63.	Duka la vifaa vya maabara	20,000
64.	Maabara ya Vipimo	20,000
65.	Zahanati	50,000
66.	Kituo cha Afya	70,000
67.	Madawa asilia	10,000
68.	Wafanyabiashara wadogo kwa siku	500
69.	Hospitali	100,000
70.	Kliniki/Herbalist	50,000
71.	Hospitali ya Rufaa	400,000
72.	Vyuo kwa safari/trip	180,000
73.	Shule ya sekondari, shule ya msingi	80,000
74.	Kituo cha kulelea watoto	60,000
75.	Kituo kikubwa cha mafuta (zaidi ya Pump 6) na service staton	200,000
76.	Kituo kidogo cha mafuta (pump 1-5) na service station	150,000
77.	Kituo cha mafuta bila service station	100,000
78.	Kituo cha mafuta ya taa	20,000
79.	Biashara ya kuuza/kufatulia tofali	80,000
80.	Kituo cha Kuuzia gesi	20,000
81.	Kibanda cha Kuuzia mkaa wa jumla	30,000
82.	Kibanda cha Kuuzia Mkaa wa rejereja	40,000
83.	Msikiti au Kanisa bila ya kuwa na shughuli nyingine za Kibiashara	3,000
84.	Msikiti au Kanisa ukiwa na shughuli nyingine za Kibiashara	50,000
85.	Jumba la Starehe/ Klabu/cassino/night clubs	250,000
86.	Ofisi za ulinzi	20,000
87.	Tax kwa siku	500
88.	Ofisi za tiketi za mabasi na kuhifadhi mizigo	50,000
89.	Daladala kwa siku	1,000
90.	Minara ya simu na mawasiliano mengine	30,000
91.	Kituo cha transformer ya umeme (Electric transformer stations)	100,000
92.	Taka za bustani kwa mita mraba moja	10,000

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

93.	Taka ngumu toka viwandani vikubwa kwa safari/tripu	350,000
94.	Taka ngumu toka viwandani vya kati kwa safari/tripu	250,000
95.	Taka ngumu toka viwandani vya kati kwa safari/tripu	180,000
96.	Taka za masoko kwa safari/tripu	300,000
97.	Ghala (Godown)	100,000
98.	Duka la vifaa vya muziki	40,000
99.	Duka la CD na cassette	10,000
100.	Bahati Nasibu	20,000
101.	Taka za Biashara kwa tripu (Super market hyper market na nyinginezo)	200,000
102.	Taka za uvunjaji wa jengo kwa tani moja (demolition debris per ton)	50,000
103.	Kituo cha kuchakata taka (wase recycling center)	60,000
104.	Night club	250,000
105.	Pooltable	10,000
106.	Gereji	120,000
107.	Fundi simu na radio	10,000
108.	Duka la vipodozi	20,000
109.	Wakusanyaji na wauzajiwa chuma chakavu	120,000
110.	Wauzaji wa oil chafu	240,000
111.	Wanaouza mairi mapya	180,000
112.	Kukata na kuuza mairi chakavu	120000
113.	Wakusanyaji na wauzaji wa chupa za plastic	60,000
114.	Wauza kuni	30,000
115.	Mawakala wapokeaji madafu madafu	120,000
116.	Wauza miwa mizima	120,000
117.	Ukumbi wa starehe	100,000
118.	Baa na ukumbi	150,000
119.	Baa na nyumba ya wageni	100,000
120.	Wauza juisi ya miwa	60,000
121.	Pikipiki (boda na bajaji) kwa siku	500
122.	Open lorry Tani 10 - 18	250,000
123.	Compactor	350,000 – 400,000

JEDWALI LA PILI

UPANDAJI MITI

Limetungwa chini ya Kifungu cha 41 (2)

Ujazo wa Juu (high density)	Miti isiyo pungua 2
Ujazo wa kati (Medium density)	Miti isiyo pungua 4
Ujazo wa chini (Low density)	Miti isiyo pungua 6

JEDWALI LA TATU

KUFIFILISHA KOSA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 51)

Mimi..... nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele yaambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwamba mnamo tarehe.....ya mwezi.....mwakanilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu chacha Sheria Ndogo za (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke za mwaka 2022.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe...ya mwezi.....Mwaka.....

Jina.....

Saini.....

Mbele ya:

Jina.....

Cheo.....

*Sheria Ndogo Za (Afya, Usafi Na Usimamizi Wa Mazingira) Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke*

Tangazo La Serikali Na.. 588 (Linaendelea)

Saini.....

Tarehe:

Lakari ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitiwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kilichofanyika tarehe 21 mwezi wa 03 mwaka 2022

ELIHURUMA SAMWEL MABELYA

Mkurugenzi

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

ABDALLAH SAID MTINIKI

Mstahiki Meya

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

NAKUBALI



Dodoma

19 Septemba, 2022

INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB)

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala

Mikoa na Serikali za Mitaa